

30 Juni 2017

## **MAPENDEKEZO YA WADAU KWENYE MISWAADA MIPYA YA MADINI-2017 YAZINGATIWE**

Sisi HakiRasilimali-PWYP, jukwaa la Asasi za Kijamii ambazo zinashughulikia masuala ya madini, mafuta na gesi nchini Tanzania, tumefuatilia kwa umakini miswada mipya ya madini iliyosomwa kwa mara ya kwanza bungeni tarehe 29 Juni 2017.

Miswada iliyosomwa kwa mara ya kwanza bungeni hapo ni:

1. Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017.
2. Muswada wa Sheria ya Mamalaka ya nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017.
3. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2017.

Tanzania ni nchi mojawapo Afrika zilizoanzisha maboresho katika sekta ya madini na harakati hizi nchini zilianza mwaka 2008 ambapo tume ya Raisi ya kupitia sekta ya madini iliyoongozwa na Jaji Mark Bomani ilitoa ripoti yenye mapendekezo mbali mbali ya kunasua sekta ya madini kwa manufaa ya wananchi wake.

**TUNAIPONGEZA** serikali kwa uamuzi wa kuwasilisha bungeni miswaa hii tajwa hapo juu Na kwa uthubutu na msimamo wa kuuhisha mjadala wa kitaifa kuhusu usimamizi wa rasilimali za nchi na manufaa yake kwa taifa.

Ni matumaini yetu kuwa mambo yafuatayo yatazingatiwa ili kuleta mjadala wenye usawa ambao utapelekea kuwepo kwa sheria nzuri ya madini ambayo inalinda maslahi ya taifa na watanzania wote kwa ujumla.

Tunaiomba Bunge la Tanzania kuhakikisha mambo yafuatayo yanazingatiwa:

1. Kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa miswaada hii, Bunge litumie muda wake wa kutosha kujiridhisha na kuepuka kupitishwa miswada kwa haraka haraka na tunapendekeza kuwepo na wigo mpana wa kufanya mashauriano na wadau wengine husika.
2. Ili kukwepa kutunga sheria zisizo na maslahi kwa wa Tanzania au sheria mbovu, tunapendekeza maoni ya wananchi yatakayowasilishwa na wawakilishi wao siku ya Jumamosi tarehe 1 Julai na Jumapili Julai 2, 2017 yajumuishwe katika miswada hii.
3. Miswada hii ya madini inatakiwa kuwa ni suala la kitaifa hivyo kutokuegemea chama chochote cha siasa au maslahi mengine kwani kwa kufanya hivyo kutakandamiza mawazo ya mtu mmoja mmoja baina ya wabunge.
4. Uzoefu umeonesha kuwa mjadala muhimu imekuwa ikipuuzwa pale ambapo miswada ya aina hii inapowasilishwa kwa hati ya dharura hivyo kuzuia uchangiaji wa kina. Sheria nzuri zenye kujali maslahi ya taifa zinatakiwa kupitishwa baada ya wadau wote muhimu kuhusishwa. Kwa siku zijazo utekelezwe mpango wa mazungumzo na wananchi katika

mihadhara juu ya sekya nzima ya uziduaji kusaidiana na asasi huru za kiraia katika maeneo ya ipatikanapo madini, gesi na mafuta.

Imesainiwa kwa niaba ya HAKIRASILIMALI-PWYP

Racheal Chagonja

Maratibu-HakiRasilimali